# Vipengele Muhimu kwenye Uanzishaji wa Majukwaa ya Kuratibu Ulinzi wa Mtoto katika kukabiliana na COVID-19

Aprili 2020

| | Kumbukumbu & zana zilizochaguliwa |
|---|---|
| 1. **Lengo:** Kuimarisha au kuanzisha jukwaa lililoundwa ili kuimarisha au kuunga mkono mamlaka za kitaifa katika kuratibu juhudi zote za kibinadamu za kulinda usalama na ustawi wa watoto dhidi ya athari zilizo na zisizo za moja kwa moja za COVID-19. Njia ya uratibu inapaswa kuimarisha uwezo wa mamlaka za kitaifa katika kutoa msaada wa kibinadamu madhubuti na ulioboreshwa, kuhakikisha ulinzi wa mtoto (CP) umejumuishwa katika sekta zote zinazohusika kama sehemu muhimu ya kukabiliana na janga, kutambua mahitaji na kuziba mapungufu ya muhimu, na kusaidia kuimarisha ubora na uwajibikaji kwa ujumla wa juhudi za pamoja. | Viwango vya chini vya Ulinzi wa watoto katika hatua za usaidizi wa kibinadamu, Kiwango cha 1 |
| 2. **Muundo:** Uanzishaji wa majukwaa ya uratibu unapaswa kulenga kuimarisha mbinu za kitaifa na tume za uratibu zilizooanzishwa, kuepuka kujirudia na uanzishaji wa mifumo inayo fanana.<br><br>Katika maeneo ambapo kuna usanifu rasmi wa kimataifa wa kibinadamu (Unaongozwa na Mratibu wa Kibinadamu, UNHCR au mipangilio mingine kwa ajili ya maeneo yaliyo changanyika), Makundi ya uratibu wa ulinzi wa mtoto yanapaswa kuunganishwa na kuelezwa kama inavyohitajika, kwa kufuata mpango kazi wa kimfumo wa kuongeza uanzishaji wa kamati za kudumu za asasi mbalimbali (IASC) kwa ajili ya COVID-19. Kama hakuna mfumo rasmi wa uratibu ulioanzishwa, taasisi na mashirika yanayo shughulikia ulinzi wa mtoto yanapaswa kubainisha mifumo iliyopo inayohitaji kuimarishwa ili kutoa huduma za uratibu kwa ufanisi. Pale inapowezekana, taasisi kuu za kitaifa zinazohusika na ulinzi wa watoto inapaswa kuwa na jukumu lakuongoza kikundi pamoja na shirika la ulinzi wa watoto lenye utaalamu wa kiufundi kwenye masuala ya ulinzi wa mtoto katika dharura na uratibu. Uwezo wa kushawishi na kuratibu pamoja na sekta zinazohusika na asasi za serikali zinazohusika katika makabiliano ni wamuhimu pia. Mifumo inapaswa kuendana na muongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kwa mashirika ya Umoja wa Mataifa yaliyo nchini na washirika ili kutengeneza mipango ya kitaifa ya kujiandaa na kukabiliana (PRP- angalia kiunga pembeni). | Mkakati wa kujiandaa na mpango wa kukabiliana wa WHO, Nguzo ya kwanza.<br><br>Mpango wa Usaidizi wa Kibinadamu wa Dunia juu ya COVID-19, uk.29-30<br><br>Mpango kazi wa Uanzishwaji wa itifaki za ukuzaji wa Kamati za Kudumu za Mashirika mbalimbali zilizo boreshwa kulingana na COVID-19 (kiunga bado hakipo)<br><br>Kitabu cha Uratibu wa Ulinzi wa Mtoto Katika Dharura, uk.19-20 |
| 3. **Vitu vya Msingi vya Kuzingatia:** Zingatia mambo haya wakati wa kuimarisha au kuanzisha kikundi cha uratibu: uanachama na makubaliano ya wajumbe (uk.43- kiunga kipo pembeni); kufuatwa kwa kanuni za utoaji huduma za kibinadamu na kanuni za ushirikiano (uk.122); kuunganisha/kusaidia au kuanzisha mifumo ya uratibu chini ya ngazi ya kitaifa (uk.41); wafanyakazi na rasilimali zingine zinazohitajika kwa ajili ya uratibu; majukumu na uwajibikaji (uk.121); mkakati wa kutoka katika ngazi ya kitaifa. | Kitabu cha Uratibu wa Ulinzi wa Mtoto Katika Dharura |
| 4. **Hatua:** Katika nchi ambapo kuna mfumo rasmi wa msaada wa kibinadamu wa kimataifa, uongozi wa mfumo huo na jukwaa lake linalohusika (muunganiko wa mashirika ya ulinzi wa watoto na viongozi wa mashirika yote katika muunganiko kwa mfano) wana uwezo wa kuanzisha kikundi maalumu cha Ulinzi wa mtoto. Pale ambapo hakuna kikundi kama hicho, serikali husika inaweza kuomba msaada wa kimataifa kukabiliana na hali ya dharura na kuanzisha vikundi vya uratibu, mara nyingi kwa ajili ya kipindi cha muda mfupi. Sheria za kitaifa juu ya milipuko ya magonjwa unaweza pia kuwepo au kutengenezwa ambao utatoa muongozo wa uratibu. | Miongozo ya mipango ya uendeshaji kusaidia maandalizi na kukabiliana kwa taifa, angalia hatua zinazofuata na Ngizo ya kwanza |
| 5. **Vitendo:** Fafanua malengo, wigo na njia za kazi katika masharti ya marejeleo yanayo eleweka kwa ajili ya kikundi. Teua mratibu (ikiwezekana na waratibu wenza), hakikisha kikundi kina uwezo wa kutoa matokeo ya taarifa za uchambuzi zinazohusika. Wajumbe wanapaswa kuweza kutenga muda kwa ajili ya mikutano (mara mbili kwa mwezi au kama itakavyo kubaliwa na kikundi), kwa ajili ya kukusanya na kushirikishana takwimu zinazo husika na kwa ajili ya kuunda kazi maalumu kama itakavyo hitajika. | Mfano wa taratibu za marejeleo ya umoja wa vikundi vilivyoundwa (halisi na isiyo halisi) inayoweza kutumika |

| | |
|---|---|
| 6. Kazi Kuu na Zana: Majukumu makuu ya vikundi vya uratibu na zana zitumikazo kikawaida katika utendaji zimeainishwa hapa chini (uratibu sio lengo linalojitegemea). Hizi zinaweza zikaongezewa, kutumiwa au kubadilishwa na mifumo iliyopo katika nchi mbalimbali. Kumbuka kwamba taasisi za kitaifa zinaweza kuwa na zana zao binafsi, katika maeneo kama usimamizi wa taarifa na uchambuzi. | Viwango vya chini vya Ulinzi wa watoto katika hatua za usaidizi wa kibinadamu, kiwango cha kwanza<br><br>Kitabu cha Uratibu wa Ulinzi wa Mtoto Katika Dharura, Kipengele cha Tatu |

| Majukumu Makuu | Zana za Kawaida (zinazo weza kubadilika) |
|---|---|
| ***i. Kusaidia utoaji wa huduma:*** Kuweka jukwaa la uratibu kutengeneza mifumo ya kutambua mapungufu na kuepuka kujirudia. | Kuorodhesha uwezo, 4W (nani anafanua kipi, wapi na wakati gani), kalenda ya matukio, vikao. |
| ***ii.Kuhusika katika ufanyaji maamuzi wa kimkakati*:** Kutambua mahitataji na mapungufu na kuchambua muktadha na hali iliyopo ili kuweka kipaumbele katika kupatia ufumbuzi. | Mfumo wa utambuzi na uchambuzi wa mahitaji (NIAF) ulioboreshwa kwa ajili ya COVID-19 (angalia muongozo hapa hapa). |
| ***iii.Kupanga na kutekeleza mipango ya kukabiliana***: tengeneza au rejelea mipango ya kisekta kama ilivyoamuliwa na muktadha wa COVID-19 na viashiria, tumia viwango vya ufundi na elezea mahitaji ya ufadhili. | Mpango wa kukabiliana wa Ulinzi wa Watoto, PRP, Mpango wa kukabiliana wa msaada wa kibinadamu, (HRP), mapendekezo ya miradi/hatua zilizopewa kipaumbele prioritized projects/actionsza kufadhiliwa + Viwango vya chini vya Ulinzi wa Watoto katika hatua za Kibinadamu kwa ajili ya viwango vya kiufundi na muongozo wake kwa ajili ya mlipuko wa magonjwa ya kuambukiza (au viwango vingine vya kitaifa). |
| ***iv.Kufuatilia na kutathmini utendaji:*** Kuangalia mabadiliko ya mahitaji, ya mwitikio (ufikiaji na ubora) na utendaji wa huduma za uratibu. | - Kufuatilia matokeo: 5w, ufuatiliaji wa shughuli, ripoti za matukio, uhakiki wa ubora (huru, binafsi au wenyewe kwa wenyewe).<br>- Ufuatiliaji wa hali: Mapitio ya Takwimu zilizochapishwa, na asasi au na jamii au na mtu wa nje).<br>- Ufuatiliaji wa Utendaji wa Uratibu (ufuatiliaji wa Utendaji wa Uratibu wa Pamoja). |
| ***v.Utetezii*:** Tambua wasiwasi na changia katika mawsiliano ya kimkakati na habari na ujumbe muhimu. | Mpango wa utetezi, jumbe za msingi za kawaida common na zana za mawasiliano (mf. picha, vidokezo, uchambuzi wa fedha). |
| ***vi.Jenga uwezo katika kujiandaa na mipango ya dharura***: Kuchangia katika uundaji wa mpango wa kitaifa wa dharura, kuuboresha na kuhakisha matumizi sahihi, na mafunzo. | Maandalizi ya kukabiliana na dharura ya milipuko ya kiafya na madhara yake + mafunzo (Kutambua mahitaji ya msingi na kuanzisha mpango wa kuyahudumia). |
| ***vii.Uwajibikaji kwa watu walioathirika:*** Wahimize wajumbe kuwajulisha na kuwahusisha watu walioathirika katika kufanya maamuzi (ikiwemo watoto), kubaliana juu ya utaratibu wa kupokea, kuchunguza na kuchukua hatua dhidi ya malalamiko, na kubaliana juu ya hatua za kuzuia ukatili na unyanyasaji wa kingono. \ | Simu za msaada kwa watoto, utaratibu wa kutoa mrejesho, ushiriki katika ufafanuzi wa programu, ushiriki wa wanajamii, kanuni za mwenendo, n.k. |

7. Vipaumbele baada ya uanzishaji: Vipaumbele vya vikundi vya uratibu ni maalumu kulingana na muktadha na vinaweza kuelezewa kuligana na sekta kwa kutumia Mfumo wa Utambuzi na Uchambuzi wa Mahitaji. Hata hivyo, hizi ni vipengele vya kawaida vinavyo onekana katika hatua za mwanzo za makabiliano vinavyopaswa kuzingatiwa: **Vipaumbele**: Rejelea mipango na uweke vipaumbele upya kwenye hatua kwa watoto walio katika mazingira hatarishi zaidi kulingana na uchambuzi mpya wa hatari; **Muendelezo na uboreshaji wa huduma**: Ongeza huduma za muhimu za ulinzi wa watoto ikiwa ni pamoja na huduma zisizo za COVID-19, tafuta washirika wa kukusaida na watendaji wengine wa ulinzi mf. Ukatili wa kijinsia ; rejelea na sisitiza mifumo iliyorekebishwa ya rufaa, ; **Utetezi wa Ulinzi wa Watoto**: kuleta mtazamo nyeti wa Ulinzi wa Watoto katika mipango na huduma za sekta zingine, na kubainisha changamoto kwa watoto na walezi walio katika hatari ya kukosa usaidizi; **Msaada katika maeneo husika**: jikite katika kusaidia watendaji katika ngazi ya chini na kuibua changamoto za msingi zilizo katika ngazi ya chini; **Kujitayarisha:** Kutambua na kujitayarisha na kukabiliana na madhara ya dharura (haswa hatari zinazohusiana na hatua za serikali za kuzuia kusambaa kwa mlipuko wa virusi na madhara ya kijamii na kiuchumi ya janga).

8. Muingiliano wa Sekta mbalimbali katika kazi: Kushiriki katika kuunda au kuhakiki kwa pamoja huduma zitolewazo na sekta zingine (haswa afya, elimu, maji na usafi, usalama wa chakula na malazina kupitia uwekaji kipaumbele kwa watu na maeneo, kwa ajili ya kutoa huduma kwa pamoja kwa watoto walio hatarini. Kuratibu tathmini na kutengeneza uchanganuzi wa sekta mbalimbali. Fanya kazi na sekata zingine kuhakikisha huduma na programu zao (i) zinapatikana kwa makundi yaliyo katika mazingira hatarishi zaidi (ikihusisha watoto wenye ulemavu); (ii) zinatolewa katika njia zilizoboresha na salama kwa watoto; (iv) haleti madhara yoyote yasiyotarajiwa; (v) zinachangia katika matokea maalumu ya ulinzi wa watoto. Tazama nguzo ya 4 ya Viwango vya chini vya Ulinzi wa watoto kwa taarifa zaidi.

9. Saidia: Eneo linalowajibika na Ulinzi wa watoto duniani inatoa usaidizi kwa vikundi vya uratibu wa ulinzi wa watoto katika muktadha wa msaada wa kibinadamu. Katika mfumo wa COVID-19, inasaidia pia njia za uratibu wa kisekta pamoja na asasi inayoongoza sekta (UNICEF katika Ulinzi wa Mtoto). Kufanya hivyo, wajumbe wa makundi ya uratibu wanaofanya kazi katika Ulinzi wa Watoto wanaweza kuwasiliana na dawati la msaada kwa lugha yao (kwa Kiarabu, Kiingereza, Kihispania na Kifaransa) kuuliza maswali ya kiufundi au kuomba mifano maalumu ya taifa ya kusaidia kazi zao. Vikundi vipya na waratibu wanaweza pia kuwasiliana na wahusika katika kanda zao kwa ajili ya kuwasiliana mtandaoni juu ya huduma zitolewazo katika ngazi ya kidunia. Eneo linalowajibika na Ulinzi wa watoto duniani ina wataalamu maalimu juu ya mada mbalimbali kama ukatili wa kijinsia, afya ya akili na msaada wa kisaikolojia, ujanibishaji, kuzuia ukatili dhidi ya watoto, uchambuzi wa kimkakati, uratibu na usimamizi wa taarifa.

Orodha ya rasilimali za COVID-19 kwa ajili ya watendaji wa Ulinzi wa Watoto inapatikana katika viungo kwenda kwenye nyenzi mpya katika mada tofauti tofauti zinazoandaliwa na kusambazwa na vikundi vya uratibu ulimwengunu. Tafadhali hakikisha unashirikisha nyenzo ulizo nazo kwa dawati letu la msaada ili kuhamasisha wenzako katika nchi zingine. **Angalia jinsi ya kuwasiliana na Eneo linalowajibika na Ulinzi wa Mtoto na upate orodha ya nyenzo za COVID19 kwa kufuata vioungo vilivyo pembezoni.**

Chaguzi za msaada wa nje kwa ajili ya Vikundi vya Uratibu katika ngazi ya Taifa kutoka kwa Eneo linalowajibika na Ulinzi wa watoto Duniani

Eneo linalo wajibika na Ulinzi wa watoto: Orodha ya rasilimali za Ulinzi wa Mtoto kwa ajili ya COVID-19